**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, IKULU KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**MEI, 2025**

**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

70 Barabara ya Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, IKULU KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika;** kwa unyenyekevu mkubwa tunamshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia afya njema na wepesi wa fikra katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku, fikra hizi zimetuwezesha kukamilisha kazi hii muhimu kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika;** kamati inatoa shukrani za dhati kwako wewe binafsi na Baraza lako Tukufu kwa kutuongoza vyema katika shuhguli zetu za kila siku kwa kutuwekea mazingira wezeshi yaliyowezesha utekelezaji wa kazi za kamati kwa ari na ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** kamati pia, inachukua fursa hii kumpongeza na kumtakia siha njema Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake wenye dhamira ya dhati ya kuwaletea wananchi maendeleo kupitia uwekezaji mkubwa wa miundombinu alioufanya pamoja na kutekeleza miradi ya kimkakati ambayo imekuza kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. Aidha, kamati inampongeza Mhe. Rais ameendelea kuonesha uongozi madhubuti uliotukuka kwa kuaminiwa na chama chake na kuteuliwa kuwa mgombea wa urais wa Zanzibar, pamoja na kupata ridhaa kubwa kutoka kwa wananchi kupitia ushindi wa kishindo wenye wingi wa asilimia katika uchaguzi. Ushindi huo ni ishara ya imani kubwa waliyonayo wananchi kwa uwezo wake wa kuiongoza Zanzibar katika misingi ya maendeleo, amani na mshikamano wa kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hakika, katika kipindi cha uongozi wake ameonesha dhamira ya dhati ya kuimarisha utawala bora na uwajibikaji ndani ya taasisi za Serikali pamoja na kusimamia matumizi sahihi ya rasilimali za umma. Hatua hizo zimechangia kuongeza imani ya wananchi kwa Serikali yao na kuimarisha ushirikiano mzuri kati ya Zanzibar na washirika mbalimbali wa maendeleo. Aidha, juhudi zake zimeendelea kufungua fursa za maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hali inayowapa wananchi matumaini makubwa kwa mustakabali bora wa Zanzibar

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi hiki kazi ya msingi ya kamati hii ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya wizara husika juu ya mapato na matumizi ya kila mwaka kama inavyoonekana katika *Kanuni ya 119* ya kanuni za kudumu ya Baraza la wawakilishi, *toleo la mwaka 2024* kupitia jadweli la kwanza kwenye majukumu ya kamati za kisekta.

**Mheshimiwa Spika;** kipekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wa kamati yangu kwa ushirikiano wao na mchango wao mkubwa waliouonesha katika upitiaji wa kazi hii. Sasa kwa ruhusa yako, naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Aza Januar Joseph | MakamuMwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Mahfoudh Abdalla Salum | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Masoud Amour Masoud | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mahmoud Shineni Ali | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Mmanga Mohamed Hamed | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *9.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *10.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *11.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

12. Ndg. Hassan Lila Mrisho Afisa Bajeti

**Mheshimiwa Spika;** kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais Ikulu kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambapo imeonesha utekelezaji wake ulikua bora kwa kuzingatia maslahi ya taifa. Sambamba na hilo, kamati imefanya uchambuzi wa malengo na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka fedha 2026/2027 kwa mnasaba na malengo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025/2030.

**Mheshimiwa Spika;** uchambuzi uliofanyika wa bajeti ya wizara hii uligusa maeneo yafuatayo:

a) Uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita (2025/2026); na

b) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika;** katika kukidhi masharti ya kanuni za kudumu ya Baraza la Wawakilishi, toleo la 2024 kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa miezi tisa ambayo iliuchambua kwa kina utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais Ikulu, sambamba na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka mpya wa fedha 2026-2027. Ripoti hiyo, ilijumuisha mpango wa bajeti kwa fungu 001- Afisi ya Rais Ikulu, fungu - 040 Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, fungu 057 - Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu na fungu 058 - Taasisi ya Afisi ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini.

**Mheshimiwa Spika;** katika **fungu 001 ya Ofisi ya Rais Ikulu** lenye programu kuu ya utawala na uendeshaji ambalo lina lengo la kuimarisha ufanisi na uratibu wa shughuli za Afisi ya Rais, Ikulu na Usalama wa Serikali, Kamati inaipongeza Afisi kwa kutekeleza vyema shuhguli zake na kuhakikisha watendaji wake wametekeleza majukumu yao kwa ubora na ufanisi. Aidha, kamati inampongeza Mhe. Rais kwa tamko lake kuongeza mishahara ya watumishi katika robo ya tatu ya bajeti ya mwaka 2026/2027 ambapo matarajio ya kamati yangu ni kunufaika kwa mtumishi wa Serikali kupitia agizo hilo. Mbali na hayo, katika utekelezaji wa programu ndogo ya

S0104 - Usimamizi wa shughuli za Afisi ya Rais Ikulu, kamati inashauri Serikali kuangalia kwa kina maslahi ya watumishi wa Ikulu katika nyongeza ya mishahara ambayo imetajwa kutokana na unyeti wa majukumu yao ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika;** kwa upande wa programu kuu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi; programu hii inategemewa kuinufaisha Zanzibar kwa kupata fursa za kiuchumi na kijamii zinazotokana na jumuiya za kikanda na kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kwa kuwekeza na kunyanyua uchumi wa taifa letu. Kwa mantiki hiyo, kamati inasisitiza kwa Serikali kuanzisha na kuimarisha mifumo ya mawasiliano ya kidijitali itakayowaunganisha wanadiaspora na taasisi za Serikali ili kupata taarifa sahihi na kwa wakati. Uwezeshaji wa mifumo hiyo utasaidia wanadiaspora hao kuwekeza nchini bila ya vikwazo vya kiutawala na kusaidia kupunguza urasimu na gharama zisizo za lazima.

**Mheshimiwa Spika;** kwa kuwa Afisi ya Rais Ikulu inajukumu la kuratibu ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano ya kikanda na kimataifa, jukumu ambalo inazijumuisha sekta mbali mbali nchini kushiriki katika mikutano na makongamano ya kimatiafa kwa lengo la kuitangaza na kuisaidia Zanzibar kupata fursa zaidi za kiuchumi na kijamii kwa maslahi ya wazanzibari. Aidha, kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu kwa taasisi ambazo zinashiriki katika mikutano na makongamano hayo ya kimataiafa kwa kupatiwa rasilimali fedha na wataalamu ambao wataweza kuishauri vizuri Serikali kutokana na matokeo ya mikutano hiyo.

**Mheshimiwa Spika;** hata hivyo, kwa kutambua na kuthamini michango ya wana diaspora, kamati inapendekeza Serikali kuweka utaratibu wa kuutambua rasmi mchango ya wana diaspora hao katika majukwaa ya kimataifa, sambamba na uhamasishaji wa diaspora kuwekeza katika sekta mbali mbali hapa nchini ikiwemo sekta ya viwanda, elimu, afya na miundombinu.

**Mheshimiwa Spika;** kwenye **fungu 040 la Baraza la Mapinduzi,** kamati inatambua kuwa ndio mhimili muhimu wa utendaji wa Serikali kwani ndilo linaloratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Serikali kwa lengo la kuleta maendeleo kwa wananchi. Kufuatia Programu Kuu ya Uratibu wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria Baraza la Mapinduzi yenye lengo la kuimarika kwa sera, sheria na miongozo yenye kusaidia ukuaji wa uchumi, maendeleo na uwajibikaji kwa watumishi wote. Kamati imeridhika na utekelezaji mzuri wa majukumu ya BLM sambamba na kuzisaidia taasisi za umma kutekeleza kikamilifu majukumu yake. Aidha, kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya usimamizi wa majukumu ya taasisi za umma katika kulinda na kuendeleza uwajibikaji kwa maslahi ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika; fungu 057 - Ofisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa;** katika programu kuu ya usimamizi wa nyaraka na kumbukumbu kwa matumizi ya taifa yenye lengo la kusimamia nyaraka na kumbukumbu zote za taasisi za serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa taaaisi zake zilizopo Zanzibar. Kupitia programu ndogo ya **S0201** - uhifadhi na utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu kwa matumizi ya Taifa, kamati inaendelea kutoa mkazo juu ya umuhimu na unyeti wa taasisi hii katika kutunza kumbukumbu za taifa na kuiomba Serikali kuongeza nguvu ya kifedha na wataalamu kwa lengo la kuwekeza katika teknolojia ya kisasa ya uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu kwa matumizi ya Serikali na kuwapa fursa watafiti kuzitumia kwa njia rahisi,sambamba na kusaidia wananchi kuwa na uelewa juu ya maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kadhalika, kamati kupitia programu kuu ya Utawala na Uendeshaji; inaendelea kuhimiza wizara juu ya umuhimu wa kukamilishwa kwa ujenzi wa jengo la taasisi ya nyaraka Kilimani ili liweze kukamilika kwa wakati uliopangwa kutokana na uhaba wa nafasi ya ofisi na matumizi makubwa ya teknolojia. Kamati pia, inaishauri Serikali baada ya kukamilisha ujenzi wa afisi kuu ya nyaraka Unguja sasa ifikirie na ujenzi wa Afisi ya Nyaraka kwa upande wa Pemba kutokana na changamoto ya ufinyu wa nafasi ambao umekuwa ukirudisha nyuma utekelezaji wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya Taasisi hii kupata mafanikio mbali mbali katika utekelezaji wa majukumu yake lakini bado zipo changamoto zinazoikabili taasisi hii ikiwemo; uhaba wa wataalamu wenye ujuzi wa kisasa, pamoja na uelewa mdogo katika baadhi ya taasisi kuhusu umuhimu wa utunzaji sahihi wa nyaraka. Kwa kuliona hilo, kamati inaendelea kutoa wito kwa Serikali kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi mbali mbali juu ya umuhimu wa uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu, pamoja na kuajiri, kuendeleza wataalamu na kuimarisha miundombinu ya kuhifadhia nyaraka hizo.

**Mheshimiwa Spika;** kupitia ***fungu 058 - Taasisi ya Afisi ya Rais ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini,*** kamati imejionea kuwa taasisi hii ina jukumu muhimu la kuhakikisha ahadi, mipango na vipaumbele vya Mheshimiwa Rais vinatekelezwa kwa ufanisi na kwa wakati. Hata hivyo, kupitia **Programu Kuu ya Mipango ya Miradi ya Kipaumbele ya Uendeshaji** yenye lengo la kuandaa mipango ya taasisi hii na uendeshaji wake ili kuweza kutekeleza shughuli zake kiuweledi. kamati inazishauri taasisi zote za Serikali kuhakikisha zinatoa mashirikiano ya moja kwa moja juu ya taasisi hii ambayo lengo lake lipo wazi kwa maslahi ya nchi yetu.

**HITIMISHO;**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia, napenda kuchukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni machache sana ya Kamati yangu, kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, nihitimishe kwa kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili waichangie, wairidhie Bajeti hii na hatimae waiidhinishie Ofisi ya Rais Ikulu, Makadirio ya Mapato na Matumizi Fedha zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha *2026/2027* ili wapate kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ***Naunga Mkono Hoja na naomba kuwasilisha.***

Ahsante,

..............................................

(**Aza Januar Joseph**)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR